JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**



Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0755675356**

**Mkuu wa Shule 0755675356**

**Makamu Mkuu wa Shule 0621919319**

**Patron 0762084165**

**Shule ya Sekondari Emanuel Nchimbi**

**S.L.P. 633**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**

**………………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**……………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI EMANUEL NCHIMBI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA MKOA WA RUVUMA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Emanuel Nchimbi ipo umbali wa Kilometa 7 Magharibi mwa Mji wa Songea. Usafiri wa basi kutoka kituo kikuu cha mabasi cha **Shule ya Tanga** unapatikana kwa Nauli ni Shilingi 700/= (Dala dala) kuelekea Mjini. Shuka kituo kiitwacho **MAUKI.** Hapo pana usafiri wa daladala kwa shilingi 600/= au pikipiki kwa Shilingi 1,500/=.



Scanned with CamScanner

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni suruali nyeusi mbili (2) zisizo bana zenye marinda mawili mbele na mfuko mmoja nyuma na Shati mbili nyeupe mikono mirefu na tai nyekundu moja nyembamba.

ii. Sare ya michezo kwa shule hii ni Track suti nyeusi yenye ufito mweupe miwili au mitatu, raba za michezo pea moja (1) najezi ya blue (Tshirt na bukta)

iii. Viatu vya shuleni vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na sio mchongoko.

iv. Soksi pea mbili nyeusi

v. Mkanda wa kuvalia suluari mweusi wa ngozi

vi. Sweta rangi ya dark bluu moja au zaidi.

vii. Nguo za kushindia ( suruali moja rangi ya ugolo na T shirt ya kola rangi ya bluu bahari)

viii.TANBIHI mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo yoyote ya nyumbani,anaporipoti awe amevaa sare za shule.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kutosha kwa masomo husika.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Scientific Calculator na graph pad moja kwa wanafunzi wa Geography;
v. Mashuka Jozi 2, rangi ya bluu bahari, blanket 1, godoro 1 futi 2.5 na foronya yake, chandarua 1 rangi yoyote.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, mopa 1, hard broom 1 na soft broom 1.

**2.3. Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |



Scanned with CamScanner

Michango yote iwekwe kwenye **namba 61810017203 NMB**. Jina la akaunti ni shule ya sekondari EMANUEL NCHIMBI SECONDARY SCHOOL

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni**



Scanned with CamScanner

**ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.



Scanned with CamScanner

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule .........................................................**

**Jina la Mkuu wa Shule; ALETAS N. MSHUHA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ..................................................**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755675356**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0621919319**
- **Mwandamizi Taaluma 0620360595**
- **Mwandamizi Malezi 0621529727**

KIAMBATISHO A
MEDICAL EXAMINATION FORM
SONGEA MUNICIPAL COUNCIL

EMANUEL NCHIMBI
SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 633



Scanned with CamScanner

SONGEA.

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine
Mr/Miss........................................................................................................ as to his/her physical and mental fitness for admission as a form FIVE student for the Academic year 2023/2024.

Your sincerely,

..................................................
THE HEADMASTER

The Headmaster, I have examined
Mr./Miss...................................................................as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary school education.

1. Vision with/without glasses: Right.................................... Left.....................
2. Blood pressure...............................................Hemoglobin.................................
3. Hearing..............................................................................................................
4. (a) Urine Albumen.......................................... (b) Sugar.....................................
5. (a) Venereal diseases........................................ (b) Bilharzias...........................
6. Pregnancy.........................................................................................
7. Neurosis............................................................................................
8. Is there any abnormality of;-
   (a) The heart............................................ (c) The spleen..................
   (b) Lungs.......................................................................................
9. Are there any serious disease e.g. Leprosy, Asthma, Diabetes, etc.

   ..........................................................................................................

   Date:......................................Station;..........................................................

   ..................................

   Signature of Medical Officer Designation ..................

KIAMBATISHO B

**KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi ;..........................................................................................



Scanned with CamScanner

2. Tarehe ya kuzaliwa; ................................................Mahali; ....................
3. Jina la Baba/Mlezi;...................................................Hai/amefariki;.........
4. Mahali anapoishi; Kijiji/Mji.............................. ... Wilaya..........................
   Mkoa...............
5. Kazi ya Baba/Mlezi.................................................!............................
6. Namba yake ya simu; .....................................................................................
7. Jina la Mama/Mlezi; ....................................................................................
8. Mahali anapoishi;
   Kijiji/Mji...................................Wilaya.....................................Mkoa.....
9. Kazi ya Mama/Mlezi; ...............................................................................
10. Namba yake ya simu; ..........................................................................

## NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

| NA | JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

KIAMBATISHO C

## AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU

- Mimi.............................................................................. Nakubali nafasi niliyopata katika shule ya sekondari Emanuel Nchimbi kuendelea na masomo.
- Nafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi.



Scanned with CamScanner

- Naahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema.
- Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.
- Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na Taifa kwa ujumla.

....................................................
Saini ya Mwanafunzi

Mimi..................................................................................................................................

Mzazi/Mlezi wa.............................................................................................................

nimesoma maelekezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anuani;-

..........................................................

..........................................................

Jina la Mzazi/Mlezi.......................................................................................

Mtaa..............................................................................................................

Saini ya mzazi/Mlezi.......................................................

Mwenyekiti wa Mtaa.........................................................................................

Tarehe..................................... Namba ya simu.............................................



Scanned with CamScanner